



جمعية الدعوة
حي العزيزية - الرياض

(١٠٠)
سُؤَالِ فِي جَوَابِهِ
(فِي عَقِيدَةِ التَّوْحِيدِ)



باللغة السواحلية

MASWALI (100) NA MAJAWABU

(KUHUSU ITIKADI YA TAWHIDI)

MTUNZI

SHEIKH ABDUL AZZIZ BIN MUHAMMAD SHAALAN

KIMEPITIWA

SHEIKH SALEH BIN FAWZAN AL FAWZAN

(mufti wa sasa wa Saudi Arabia)

TARJAMA

BAADHI YA WANAFUNZI WA CHUO KIKUU CHA MADINA

TARJAMA IMEPITIWA

Dr. SALIM KARARI

**(Mhitimu wa kitivo cha Daawa katika chuo kikuu cha Kiislamu cha
Madina)**

طبع على نفقة بعض المحسنين غفر الله لهم ولوالديهم وذريتهم ولجميع المسلمين



UTANGULIZI WA WAFASIRI

Kila sifa njema anastahiki ALLAH mola wa viumbe vyote, na swala na salamu ziwe juu ya Mtume wetu Muhammad. Hii ni tarjama ya risala fupi iliyobeba faida nyingi katika maudhui ya itiqadi ambayo imeandikwa kwa mtindo wa suali na jawabu lake na Sheikh Abdul Azziz Sha'alan- ALLAH amhifadhi- na amlipe kwa amali yake hii. Baada ya kukaa kwa pamoja baadhi ya wanafunzi kwa kuipitia na kuisoma, na kuiona kuwa ni risala iliyokusanya mambo mengi ya itiqadi ambayo yatakikana kila muislamu kuyatambua na kuyaitakidi. Tumeonelea kuifanyia tarjama ili kukurubisha ufahamu kwa kila mwenye kuzungumza lugha ya Kiswahili ili ujumbe uweze kumfikia kila mmoja wetu kwa wepesi, hasa hasa kwa nchi zenye kuzungumza lugha ya KISWAHILI ambazo ni **TANZANIA, KENYA, UGANDA, BURUNDI, RWANDA, JAMHURI YA KIDEMOKRASIA YA CONGO (DRC) na MSUMBIJI (MOZAMBIQUE).**

Waliofanya tarjama hii ni baadhi ya wanafunzi wa chuo kikuu cha kiislamu cha Madina Saudi Arabia (ISLAMIC UNIVERSITY OF MADINA).

Ambao ni Ndugu:

- 1) **ABUU QUTAYBA MUHAMED KHAMIS**
- 2) **ABUU HANBAL ABUU BAKAR MZEE**
- 3) **ABUUL YAMMAN AYUBU RASHID**
- 4) **ABUU MARYAM MUHAMAD SHADHIL**

Na ikapitiwa tarjama hii na: **Dr. SALIM KARARI.**

Na wingi wa shukran tunazipeleka kwa ALLAH kwa kutupa afya na uwezo wa kukamilisha tarjama hii, kisha kwa **Dr** aliyeipitia tarjama hii na kuirekebisha pale palipohitajia marekebisho ili kuiweka kwenye ufanisi uliobora zaidi. Na wala hutujidai ukamilifu kwa hilo, bali ukamilifu niwa ALLAH- aliyetakasika- pekee.

Tunamuomba ALLAH mtukufu ajaalie kazi hii iwe katika mema yake siku ya kiyama kila aliyeshiriki kuifainikisha, na pia ajaalie ni yenye manufaa kwa waislamu.

08/11/2024M (06/05/1446H)

Madina Saudi Arabia

الحمد لله وبعد:

قرأت هذه الأسئلة والأجوبة التي كتبها الشيخ عبد العزيز بن محمد الشعلان، وضمنها كتاب ((ثلاثة الأصول والقواعد الأربع)) للشيخ الإمام المجدد محمد بن عبد الوهاب رحمته الله فوجدت ذلك عملاً جيداً مفيداً يعين على معرفة هذا الكتاب الجليل، ويقربه للأفهام، فجزاه الله خيراً ونفع بعلمه.

كتبه

صالح بن فوزان الفوزان

(المفتي الحالي للمملكة العربية السعودية)

في ٢١/٣/١٤٤٠هـ

Kwa jina la ALLAH mwingi wa rehema na mwenye kurehemu

Kila sifa njema anastahiki ALLAH; Na baada ya hayo:

Nimeyasoma haya maswali na majawabu ambayo ameyaandika Sheikh Abdul Aziz bin Muhammad Sha'alan, na ameyakusanya maswali haya kwenye kitabu ((Thalaathatul Uswuul na kitabu Alqawaaidul Arbaa)) cha Sheikh,Imamu, Mujaddid wa dini Muhammad bin Abdil Wahhaab-ALLAH amrehemu-, basi nikaipata kuwa ni kazi nzuri mno tena yenye kuleta faida na inasaidia katika kufahamu kitabu hicho kitukufu (Thalaathatul Uswuul &Al qawaaidul Arbaa) na inakisogeza katika fahamu, basi namuomba ALLAH amlipe kila kheri na anufaishe kwa elimu yake.


Ameandika hayo:

Swaleh bin Fawzaan Al fawzaan

Mjumbe wa jopo la wanachuoni wakubwa (Saudi Arabia)

(mufti wa sasa wa Saudi Arabia).

Tarehe 21/03/1440H.



UTANGULIZI WA MTUNZI WA KITABU

الحمد لله رب العالمين، والصلاة والسلام على أشرف الأنبياء والمرسلين،

أما بعد:

فهذه أسئلة وأجوبتها في أصل الأصول توحيد الله سبحانه، والتحذير من ضده وهو الشرك بالله ووسائله، وفي معتقد أهل السنة والجماعة، صغتها بطريقة مختصرة، راعيت فيها أن تكون سهلة الفهم للقارئ.

أسأل الله سبحانه أن ينفع بها.

عبد العزيز بن محمد الشعلان

Kwa jina la ALLAH mwingi wa rehema na mwenye kurehemu

Kila sifa njema anastahiki ALLAH mola mlezi wa viumbe wote, na swala na salamu ziwe juu ya mtukufu wa manabii na mitume, ama baada ya hayo: Basi haya ni maswali na majawabu yake kuhusu msingi wa misingi yote ambayo ni tawhidi ya kumpwekesha ALLAH - utakatifu ni wake- na kutahadharisha kinyume cha Tawhidi nayo ni shirki ya kumshirikisha ALLAH na njia zake, na kuhusu itikadi ya Ahlus sunna waljamaa, nimeyaleta (maswali haya) kwa njia ya ufupi, nimechungu kwamba yawe ni mepesi kwa ufahamu wa msomaji.

Namuomba ALLAH -utakatifu ni wake- anufaishe kupitia maswali haya.

Abdul Aziz bin Muhammad Sha'alan .

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

س ۱: لماذا ندرس التوحيد؟

S1: Ni kwa nini tunasoma Tawhidi?

ج ۱: لأنه أصل الأصول، ومن أجله خلق الله الجن والإنس، وأرسل الله الرسل، وأنزل الكتب، وقام سوق الجنة والنار، وانقسم الناس إلى مسلمين وكفار، قال الله تعالى: ﴿وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ﴾ [الدَّارِيَات: ۵۶]

J1: Kwa sababu Tawhidi ndio msingi wa misingi yote, na kwa ajili yake Allah ameumba majini na watu, na Allah ametuma mitume, na akateremsha vitabu, na likasimama soko la Pepo na Moto, na watu wakagawanyika waislamu na makafiri, amesema Allah mtukufu: ﴿na sikuwaumba majini na watu isipokuwa waniabudu mimi﴾ [Adh-Dhariyat: 56]

س ۲: من أين نأخذ عقيدتنا؟

S2: Wapi tunachukua itikadi yetu?

ج ۲: من القرآن والسنة وما كان عليه سلف الأمة.

J2: Kutoka katika Qur'an na Sunna na yale ambayo wamekuwa nayo watu wema waliotangulia wa umati huu.

س ۳: ما الأصول الثلاثة التي يجب على الإنسان معرفتها، والتي يسأل عنها في قبره؟

S3: Ni ipi misingi mitatu ambayo ni wajibu juu ya kila mwanadamu kuijua, na ambayo ataulizwa katika kaburi lake?

ج ٣: معرفة العبد ربه، ودينه، ونبيه محمدا ﷺ.

J3: Ni mja kumjua Mola wake, na dini yake, na Mtume wake Muhammad swala na salamu ziwe juu yake.

س ٤: من ربك؟

S4: Ni nani mola wako?

ج ٤: ربي الله الذي رباني، وربى جميع العالمين بنعمه، وهو معبودي ليس لي معبود سواه، والدليل

قوله تعالى: ﴿الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ﴾ [الفاتحة: ٢]

J4: Mola wangu ni Allah ambaye amenilea mimi, na akavilea viumbe vyote kwa neema zake, na yeye ndiye muabudiwa wangu sina mimi muabudiwa asiyekuwa yeye, na dalili ya hayo ni maneno yake Allah mtukufu: ﴿Kila sifa njema anastahiki Allah mola wa viumbe wote﴾ [Al-Fatiha: 2]

س ٥: بم عرفت ربك؟

S5: Kwa jambo gani umemjua mola wako?

ج ٥: عرفته بآياته ومخلوقاته، ومن آياته: الليل والنهار، والشمس والقمر، ومن مخلوقاته:

السموات السبع ومن فيهن، والأرضون السبع ومن فيهن، وما بينهما، والدليل قوله تعالى: ﴿وَمِنْ

آيَاتِهِ اللَّيْلُ وَالنَّهَارُ وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرُ لَا تَسْجُدُوا لِلشَّمْسِ وَلَا لِلْقَمَرِ وَاسْجُدُوا لِلَّهِ الَّذِي خَلَقَهُنَّ إِن كُنتُمْ

إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ﴾ [فصلت: ٣٧]

J5: Nimemjua kwa alama zake na viumbe vyake, na miongoni mwa alama zake: ni usiku na mchana, na jua na mwezi, na miongoni mwa viumbe vyake: ni mbingu saba na vile vilivyomo ndani yake, na ardhi saba na vile vilivyomo ndani yake, na vilivyomo baina ya mbingu na ardhi, na dalili ya hayo ni maneno yake Allah mtukufu: ﴿Na miongoni mwa alama zake ni usiku na mchana na jua na mwezi, basi msisujudie jua wala mwezi bali msujudieni Allah aliyeviumba hivyo ikiwa mnamuabudu yeye tu﴾ [Fuswilat:

37].

س٦: أين الله؟

S6: Yupo wapi Allah?

ج٦: في السماء مستو على العرش

J6: Yupo mbinguni juu ya arshi.

س٧: ما الدليل من القرآن على أن الله سبحانه في السماء وهو على العرش؟

S7: Ni ipi dalili kutoka katika Qur'an juu ya kwamba Allah aliye takasika yupo mbinguni juu ya Arshi?

ج٧: الدليل أنه في السماء قوله تعالى: ﴿عَآمِنْتُمْ مِّنْ فِي السَّمَآءِ أَن يَخْسِفَ بِكُمْ الْأَرْضَ فَإِذَا هِيَ تَمُورٌ﴾ [المُلْك: ١٦]

والدليل أنه على العرش قوله تعالى: ﴿الرَّحْمَنُ عَلَى الْعَرْشِ اسْتَوَى﴾ [طه: ٥٠]. في سبعة مواضع من كتابه.

J7: Dalili yakuwa yupo juu ya mbingu ni maneno yake Allah mtukufu: ﴿Je mnajiaminisha kwa Allah aliye juu﴾. [Al-mulk:16]

Na dalili ya kuwa yupo juu ya arshi ni maneno yake Allah mtukufu: ﴿Mwingi wa rehema yupo juu ya Arshi﴾ [Twaha:5]. Imetajwa sehemu saba ndani ya kitabu chake (Qur'an).

س٨: ما معنى (استوى)؟

S8: Nini maana ya amekuwa juu?

ج٨: علا وارتفع وصعد واستقر.

J8: Amekuwa juu na amenyanyuka.

س٩: لماذا خلق الله الجن والإنس؟

S9: Kwa nini Allah ameumba majini na watu?

ج٩: لعبادته وحده لا شريك له.

J9: Kwa ajili ya kumuabudu yeye peke yake, hana mshirika.

س١٠: ما الدليل من القرآن على أن الله خلق الجن والإنس لعبادته؟

S10: Ni ipi dalili kutoka kwenye Qur'an kwamba Allah ameumba majini na watu kwa ajili ya kumuabudu yeye?

ج١٠: قوله تعالى: ﴿وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ﴾ [الدَّارِيَّاتُ : ٥٦]

J10: Ni maneno yake Allah mtukufu: ﴿Na sikuumba majini na watu isipokuwa waniabudu mimi﴾ [Adh-Dhariyat: 56]

س١١: ما معنى يعبدون؟

S11: Nini maana ya waniabudu mimi?

ج١١: يوحّدون.

J11: Wanipwekeshe mimi.

س١٢: ما العبادة؟

S12: Nini Ibada?

ج١٢: هي اسم جامع لكل ما يحبه الله ويرضاه من الأقوال والأعمال الباطنة والظاهرة.

J12: Ni jina lenye kukusanya kila kile ambacho anakipenda Allah na kukiridhia katika kauli (maneno) na matendo ya siri na ya wazi.

س ۱۳: ما معنى شهادة أن لا إله إلا الله؟

S13: Nini maana ya kushuhudia ya kwamba hapana muabudiwa isipokuwa Allah?

ج ۱۳: أي: لا معبود بحق إلا الله.

J13: Maana yake: hakuna muabudiwa wa haki isipokuwa Allah.

س ۱۴: ما معنى شهادة أن محمدا رسول الله؟

S14: Nini maana ya kushuhudia kuwa Muhammad ni mjumbe wa Allah?

ج ۱۴: طاعته فيما أمر، وتصديقه فيما أخبر، واجتناب ما نهى عنه وزجر، وألا يعبد الله إلا بها
شرع.

J14: Ni kumtii kwa yale ambayo ameamrisha, na kumuamini kwa yale ambayo ameyatolea habari, na kujiepusha na yale ambayo ameyakataza na akayakemea, na kwamba asiabudiwe Allah isipokuwa kwa yale ambayo ameyawekea sheria.

س ۱۵: ما أعظم ما أمر الله تعالى به؟

S15: Ni jambo gani kubwa ambalo Allah mtukufu ameliamrisha?

ج ۱۵: أعظم ما أمر الله به هو التوحيد، وهو عبادته وحده لا شريك له؛ قال تعالى: ﴿وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنْ أَعْبُدُوا اللَّهَ وَأَجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ﴾ [التَّحْل: ۳۶]

J15: Jambo kubwa ambalo Allah ameliamrisha ni Tawhidi (kumpwekesha Allah) nayo ni kumuabudu Allah pekee asiye na mshirika, amesema Allah mtukufu: ﴿Na kwa hakika tumetuma katika kila umma mtume awaambie watu wake muabudieni Allah na jiepusheni na twaaghuti﴾ [Annahl:36]

س ١٦ : ما أقسام التوحيد؟

S16: Ni vipi vigawanyo vya Tawhidi?

ج ١٦ : توحيد الربوبية، وتوحيد الألوهية، وتوحيد الأسماء والصفات.

J16: Tawhidi ya ulezi (*Rubuubiyah*), Tawhidi ya uungu (*Uluuhiyah*) na Tawhidi ya majina na sifa za Allah.

س ١٧ : ما تعريف توحيد الربوبية؟

S17: Nini maana ya Tawhidi ya ulezi (*Rubuubiyah*)?

ج ١٧ : إفراد الله بأفعاله، مثل: الخلق والرزق وإنزال المطر وغير ذلك.

J17: Ni kumpwekesha Allah kwa vitendo vyake, mfano: kuumba, kuruzuku, kunyesheza mvua na mengineyo.

س ١٨ : ما تعريف توحيد الألوهية؟

S18: Nini maana ya Tawhidi ya uungu (*Uluuhiyah*)?

ج ١٨ : إفراد الله بأفعال العباد التي شرعها لهم، مثل؛ الدعاء، والذبح، والسجود.

J18: Ni kumpwekesha Allah kwa vitendo vya waja wake alivyowaamrisha, mfano: kuomba dua, kuchinja, na kusujudu.

س ١٩ : ما تعريف توحيد الأسماء والصفات؟

S19: Nini maana ya Tawhidi ya majina ya Allah na sifa zake?

ج ١٩: هو أفراد الله سبحانه بما يختص به من أسماء وصفات. قال تعالى: ﴿لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ﴾ [الشورى: ١١]

J19: Ni kumpwekesha Allah aliye takasika kwa yale ambayo anahusika nayo pekee katika majina na sifa. Amesema Allah mtukufu: ﴿Hakuna kitu kama mfano wake, naye ni mwenye kusikia na kuona﴾ [Ash-Shura: 11]

س ٢٠: اذكر بعض أنواع العبادة؟

S20: Taja baadhi ya aina za Ibada?

ج ٢٠: من أنواعها: الدعاء، والاستغاثة، والاستعانة، وذبح القربان، والنذر، والخوف، والرجاء، والتوكل، والإنابة، والمحبة، والخشية، والرغبة، والرغبة، والركوع، والسجود، والخشوع، والتذلل، والذكر، وقراءة القرآن.

J20: Miongoni mwa aina za ibada: ni kuomba dua, kutaka uokovu, kutaka msaada, kuchinja vikurubishwa, kuweka nadhiri, kukhofu, kutarajia, kutegemea, kurejea (kutubia), kupenda, kunyenyekea, kupupia, kuogopa (kunako ambatana na elimu), kurukuu, kusujudu, kuwa na khushui, kujidhalilisha, dhikri (kumtaja Allah), na kusoma Qur'an.

س ٢١: ما أعظم ما نهى الله عنه؟

S21: Ni jambo gani kubwa ambalo Allah amelikataza?

ج ٢١: أعظم ما نهى عنه الشرك، وهو عبادة غير الله مع الله؛ قال تعالى: ﴿إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَنْ يَشَاءُ﴾ [النساء: ٤٨]

J21: Jambo kubwa ambalo Allah amelikataza ni shirki. Nayo ni kumuabudu asiyekuwa Allah pamoja na Allah. Amesema Allah mtukufu: ﴿Hakika ya Allah hasamehe [dhambi] ya kushirikishwa, na anasamehe dhambi iliyo chini ya shirki kwa amtakaye﴾ [An-Nisaa: 48]

س ٢٢: ما نوعا الشرك؟

S22: Ni zipi aina mbili za shirki?

ج ٢٢: النوع الأول: الشرك الأكبر: وهو كل ما سواه الله أو رسوله صلى الله عليه وسلم شركا، وأخرج صاحبه من الإسلام؛ مثل: عبادة الأصنام والأموات، والسجود لغير الله.

النوع الثاني: الشرك الأصغر: وهو كل ما جاء في الشريعة أنه شرك ولم يخرج صاحبه من

الإسلام؛ مثل: الحلف بغير الله، ويسير الرياء، وقول: ما شاء الله وشئت. وسمي شركا أصغر لأنه وسيلة للوقوع في الشرك الأكبر.

J22: **Aina ya kwanza:** Shirki kubwa: Nayo ni kila ambalo ameliita Allah au Mtume wake kuwa ni shirki, na likamtoa mfanyaji wake katika uislamu mfano: kuabudu masanamu na maiti (wafu) na kumsujudia asiyekuwa Allah.

Aina ya Pili: Shirki ndogo: Nayo ni kila ambalo limekuja katika sheria kuwa ni shirki na wala halimtoi mfanyaji wake katika uislamu mfano: kumuapia asiyekuwa Allah, na ria iliyokuwa nyepesi, na kusema: akitaka Allah na ukitaka wewe. Na imeitwa shirki ndogo kwa sababu inapelekea kwenye shirki kubwa.

س ٢٣: متى وقع أول شرك في الناس؟

S23: Ni wakati gani ilitokea shirki ya kwanza kwa watu?

ج ٢٣: وقع أول شرك في الناس في قوم نوح عليه السلام.

J23: Ilitokezea shirki ya mwanzo kwa watu, katika kaumu ya Nuhu, swala na salamu ziwe juu yake.

س ٢٤: ما سبب وقوع الشرك في قوم نوح؟

S24: Ni ipi sababu ya kutokea shirki kwa watu wa Nuhu?

ج ٢٤: السبب هو: الغلو في الصالحين.

J24: Sababu yake: ni kuvuka mipaka katika kuwatukuza watu wema.

س ٢٥: ما معنى الغلو في الصالحين؟

S25: Nini maana ya kuvuka mipaka katika kuwatukuza watu wema?

ج ٢٥: هو الزيادة في مدحهم، ورفعهم فوق مكانتهم، بأن يصرف لهم شيء من العبادة، والدليل قوله تعالى: ﴿يَا أَهْلَ الْكِتَابِ لَا تَغْلُوا فِي دِينِكُمْ﴾ [النساء: ١٧١]، وقال ﷺ: «لا تطروني كما أطرت النصارى عيسى ابن مريم، إنما أنا عبد، فقولوا: عبد الله ورسوله»، رواه البخاري. ومعنى (لا تطروني) أي: أي لا تزيدوا في مدحي.

J25: Ni kuzidisha katika kuwasifu, na kuwainua zaidi ya vyeo vyao, kiasi cha kuwageuzia sehemu katika ibada. Na dalili ni maneno yake Allah mtukufu: ﴿Enyi mliyo pewa kitabu msivuke mipaka katika dini yenu﴾

[Annisaa:171], na amesema Mtume ﷺ: ((Msizidishe katika kunisifu kama walivyo zidisha manaswara (wakristo) katika kumsifu Issa mwana wa Mariam, hakika [si vyenginevyo] mimi ni mja wa Allah, basi semeni: mja wa Allah na mtume wake)) [Ameipokea Bukhari].

Na maana ya (*tutw-runiy*), ni kwamba: Msizidishe (mkavuka mipaka) katika kunisifu.

س ٢٦: ما حكم دعاء الأموات؟

S26: Ni ipi hukumu ya kuwaomba maiti (wafu)?

ج ٢٦: دعاء الأموات وغيرهم فيما لا يقدر عليه إلا الله شرك أكبر يخرج من الإسلام؛ والدليل من القرآن: ﴿وَمَنْ يَدْعُ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ لَا بُرْهَانَ لَهُ بِهِ فَإِنَّمَا حِسَابُهُ عِنْدَ رَبِّهِ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ الْكَافِرُونَ﴾ [المؤمنون: ١٧٧]

J26: Kuwaomba maiti (wafu) na wengineo katika yale ambayo hana uwezo wa kuyafanya isipokuwa Allah pekee ni shirki kubwa ambayo humtoa mtu kwenye uislamu, na dalili kutoka kwenye Qur'an: ﴿Na anaye muomba

pamoja na Allah, mola mwingine hana hoja kwa hili; basi bila shaka hisabu yake ipo kwa Mola wake. Kwa hakika makafiri hawafanikiwi». [Al-Mu'minuun: 117].

س ٢٧: هل يحتاج دعاء الله لواسطة مخلوق؟

S27: Je inahitajia kumuomba Allah ukati na kati (uunganishi wa kiumbe)?

ج ٢٧: لا يحتاج الدعاء لواسطة مخلوق، والدليل قوله تعالى: ﴿وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ﴾ [البقرة: ١٨٦]

J27: Haihitaji dua ukati na kati wa kiumbe, na dalili ni maneno yake Allah mtukufu: ﴿Na waja wangu watakapo kuuliza kuhusu mimi, waambie kuwa mimi nipo karibu, naitikia maombi ya muombaji anapo niomba﴾. [Al-baqara: 186].

س ٢٨: هل يستجيب الأموات للدعاء؟

S28: Je maiti (wafu) wanajibu dua (maombi)?

ج ٢٨: الأموات لا يستجيبون للدعاء؛ والدليل قوله تعالى: ﴿إِن تَدْعُوهُمْ لَا يَسْمَعُوا دُعَاءَكُمْ وَلَوْ سَمِعُوا مَا اسْتَجَابُوا لَكُمْ وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ يَكْفُرُونَ بِشِرْكِكُمْ﴾ [فاطر: ١٤]

J28: Maiti (wafu) hawajibu dua (maombi), na dalili ni kauli yake Allah mtukufu: ﴿Ikiwa mtawaomba hawasikii maombi yenu, na hata wakisikia hawakujibuni, na siku ya kiyama watakanusha ushirikina wenu﴾. [Faatir: 14].

س ٢٩: لمن نذبح ونصلي؟

S29: Ni kwa ajili ya nani tunachinja na kusali?

ج ٢٩: لله وحده لا شريك له؛ قال تعالى: ﴿فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَأَنْحَرْ﴾ [الكَوْثَرُ: ٢].

J29: Ni kwa ajili ya Allah peke yake hana mshirika ; amesema Allah mtukufu: ﴿Basi sali na uchinje kwa ajili ya mola wako﴾. [Al-Kauthar: 2]

س ٣٠: ما حكم الذبح والسجود لغير الله؟

S30: Ni ipi hukumu ya kuchinja na kumsujudia asiye kuwa Allah?

ج ٣٠: شرك أكبر مخرج من ملة الإسلام. قال الله تعالى: ﴿قُلْ إِنْ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٦٦﴾ لَا شَرِيكَ لَهُ وَبِذَلِكَ أُمِرْتُ وَأَنَا أَوَّلُ الْمُسْلِمِينَ﴾ [الْأَنْعَام: ١٦٢ - ١٦٣]، (نسكي: أي ذبحي).

J30: Ni shirki kubwa, inayomtoa (mtu) katika Uislamu. Amesema Allah mtukufu: ﴿Sema ewe mtume: Hakika sala zangu, na kuchinja kwangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Allah, mola wa viumbe vyote hana mshirika, na kwa ajili ya hilo (Tawhidi) nimeamrisha, na mimi ni wa kwanza wa waislam﴾ [Al - An'aam: 162, 163]. (Nusukiy: Ni kuchinja kwangu).

س ٣١: ما حكم الحلف بغير الله؛ مثل الحلف بالنبي ﷺ أو الأمانة أو الشرف أو غيرها؟

S31: Ni ipi hukumu ya kumuapia asiye kuwa Allah; mfano kumuapia Mtume ﷺ au amana au cheo au kitu chengine?

ج ٣١: حكمه: شرك أصغر. قال ﷺ: «من كان حالفا فليحلف بالله أو ليصمت». رواه البخاري.

J31: Hukumu yake ni shirki ndogo. Amesema mtume ﷺ: ((Yule atakaye apa, basi na amuapie Allah au anyamaze)). [Ameipokea Bukhari].

س ٣٢: ما الواجب على المسلم تجاه أسماء الله وصفاته؟

S32: Ni upi wajibu juu ya Muislam upande wa majina ya Allah na sifa zake?

ج ٣٢: إثبات ما أثبتته الله لنفسه، أو أثبتته له رسوله ﷺ، ونفي ما نفاه الله عن نفسه، أو نفاه عنه رسوله ﷺ، من أسمائه وصفاته سبحانه وتعالى، من غير تحريف ولا تعطيل ولا تكييف ولا تمثيل.

J32: Ni kuthibitisha yale ambayo amejithibitishia Allah kwa nafsi yake, au amemthibitishia Mtume wake ﷺ, na kukanusha yale aliyo jikanushia Allah nafsi yake, au aliyo mkanushia Mtume wake ﷺ, miongoni mwa majina yake na sifa zake -kutakasika ni kwake Allah- pasi na kupindisha wala kukanusha wala kuweka namna (ya sifa ya Allah), wala kumfananisha.

س ٣٣: ما الدليل من القرآن على أن صفات الله لا تشبه صفاتنا؟

S33: Ni ipi dalili kutoka kwenye Qur'an juu ya kwamba sifa za Allah hazifanani na sifa zetu?

ج ٣٣: قوله تعالى: ﴿لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ﴾ [الشُّورَى : ١١]

J33: Ni kauli yake Allah mtukufu: ﴿Hakuna kitu kama mfano wake, naye ni mwenye kusikia na mwenye kuona﴾ [Ash-shuura: 11].

س ٣٤: ما دينك؟

S34: Ni ipi dini yako?

ج ٣٤: ديني الإسلام؛ والدليل قوله تعالى: ﴿إِنَّ الدِّينَ عِنْدَ اللَّهِ الْإِسْلَامُ﴾ [آلِ عِمْرَانَ : ١٩]

J34: Dini yangu ni Uislamu; na dalili ni kauli yake Allah mtukufu: ﴿Bila ya shaka dini ya haki mbele ya Allah ni Uislamu﴾ [Al- Imran: 19].

س ٣٥: هل يقبل الله ديننا غير الإسلام بعد مبعث محمد ﷺ؟

S35: Je Allah atakubali dini yoyote isiyo kuwa Uislamu baada ya kutumwa Muhammad ﷺ?

ج ٣٥: لا يقبل الله ديننا غير دين الإسلام بعد بعثة الرسول ﷺ؛ والدليل قوله تعالى: ﴿وَمَنْ يَبْتَغِ

غَيْرَ الْإِسْلَامِ دِينًا فَلَنْ يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ مِنَ الْخَسِرِينَ﴾ [آل عمران: ٨٥]

J35: Hatokubali Allah dini yoyote isiyo kuwa dini ya Uislamu baada ya kutumwa Mtume ﷺ. Na dalili ni kauli yake Allah mtukufu: ﴿Na yeyote anaye tafuta dini isiyo kuwa Uislamu haitakubaliwa kwake, naye Akhera atakuwa miongoni mwa wenye kupata hasara﴾ [Al- Imran: 85].

س ٣٦: ما تعريف الإسلام؟

S36: Nini maana ya Uislamu?

ج ٣٦: هو: الاستسلام لله بالتوحيد، والانقياد له بالطاعة، والبراءة من الشرك وأهله.

J36: Ni kujisalimisha kwa Allah kwa Tawhidi (kumpwekesha), na kunyenyekea kwake kwa kumtii, na kujiweka mbali na shirki na watu wake.

س ٣٧: ما أركان الإسلام؟

S37: Ni zipi nguzo za Uislamu?

ج ٣٧: شهادة أن لا إله إلا الله وأن محمدا ﷺ عبده ورسوله، وإقام الصلاة، وإيتاء الزكاة،

وصوم رمضان، وحج البيت من استطاع إليه سبيلا. والدليل قوله عليه الصلاة والسلام:

«الإسلام أن تشهد أن لا إله إلا الله وأن محمدا رسول الله، وتقيم الصلاة، وتؤتي الزكاة، وتصوم

رمضان، وتحج البيت إن استطعت السبيل»، رواه البخاري ومسلم.

J37: Ni kushuhudia ya kwamba hapana anaepasa kuabudiwa kwa haki ispokuwa Allah na hakika Muhammad ﷺ ni mja wake na mtume wake, na kusimamisha sala, na kutoa zaka, na kufunga mwezi wa Ramadhani, na kuhiji nyumba tukufu kwa yule mwenye uwezo wa kuendea njia hiyo. Na dalili ni kauli yake mtume ﷺ: ((Uislamu ni kushuhudia ya kwamba hapana mola anaepasa kuabudiwa kwa haki ispokuwa Allah na hakika Muhammad ﷺ ni mja wake na mtume wake, na kusimamisha sala, na kutoa zaka, na kufunga mwezi wa Ramadhani, na kuhiji nyumba tukufu kwa yule mwenye uwezo wa kufunga safari kwenda huko)). [Ameipokea Bukhari na Muslim].

س ٣٨: ما تعريف الإيمان؟

S38: Nini maana ya Imani?

ج ٣٨: هو: قول باللسان، واعتقاد بالقلب، وعمل بالجوارح، يزيد بالطاعة، وينقص بالمعصية.

J38: Ni kusema kwa ulimi, na kuitakidi kwa moyo, na kutenda kwa viungo, huzidi kwa kumtii Allah, na hupungua kwa kumuasi.

س ٣٩: ما أركان الإيمان؟

S39: Ni zipi nguzo za Imani?

ج ٣٩: الإيمان بالله وملائكته وكتبه ورسله واليوم الآخر، وتؤمن بالقدر خيره وشره. والدليل قوله عليه الصلاة والسلام: « الإيمان أن تؤمن بالله وملائكته وكتبه ورسله واليوم الآخر، وتؤمن بالقدر خيره وشره », رواه مسلم.

J39: Ni kumuamini Allah na malaika wake na vitabu vyake na mitume wake na siku ya mwisho, na kuamini kadari kheri zake na shari zake. Na ushahidi ni kauli yake ﷺ. ((Imani: ni kumuamini Allah na malaika wake na vitabu vyake na mitume wake na siku ya mwisho, na kuamini kadari kheri zake na shari zake)). [Ameipokea Muslim].

س ٤٠: من الملائكة؟

S40: Ni nani Malaika?

ج ٤٠: الملائكة عالم غيبي خلقوا من النور، خلقهم الله لعبادته.

J40: Malaika ni viumbe wa ghaibu (walio fichikana), wameumbwa kutokana na nuru, amewaumba Allah kwa ajili ya kumuabudu.

س ٤١: ما حكم الإيمان بالملائكة؟

S41: Ni ipi hukumu ya kuamini Malaika?

ج ٤١: واجب لا يقبل الإيمان إلا به.

J41: Ni wajibu (lazima), haitokubaliwa Imani isipokuwa kwa kuamini Imani hiyo.

س ٤٢: من أفضل الملائكة؟

S42: Ni nani mbora zaidi wa Malaika?

ج ٤٢: جبريل عليه السلام، وهو الموكل بإنزال الوحي.

J42: Ni Jibril amani iwe juu yake, na yeye amewakilishwa kwa kuteremsha wahyi.

س ٤٣: ما الكتب السماوية؟

S43: Ni vipi vitabu vya mbinguni?

ج ٤٣: هي الكتب التي أنزلها الله على الرسل عليهم السلام، مثل: التوراة، والإنجيل والزبور والقرآن.

J43: Ni vitabu ambavyo ameviteremsha Allah juu ya mitume amani iwe juu yao, mfano: Taurati, Injili, Zaburi na Qur'an.

س ٤٤: ما حكم الإيمان بالكتب؟

S44: Ni ipi hukumu ya kuamini vitabu?

ج ٤٤: واجب، لا يقبل الإيمان إلا به.

J44: Ni wajibu (lazima), haitokubaliwa imani isipokuwa kwa kuamini Imani hiyo.

س ٤٥: ما أعظم الكتب السماوية؟

S45: Ni kipi kitukufu zaidi katika vitabu vya mbinguni?

ج ٤٥: أعظم الكتب: هو القرآن العظيم الذي أنزله الله على محمد ﷺ وهو ناسخ لجميع الكتب السماوية، فلا يجوز التعبد لله إلا به، قال تعالى: ﴿وَأَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ الْكِتَابِ وَمُهَيْمِنًا عَلَيْهِ﴾ [المائدة: ٤٨]

J45: Kitabu kitukufu zaidi ni Qur'an tukufu ambayo ameiteremsha Allah kwa Muhammad ﷺ. Nayo ni yenye kufuta vitabu vyote vya mbinguni, haitafaa kumuabudia Allah isipokuwa kwa hiyo Qur'an, amesema Allah mtukufu: ((Na tumekuteremshia kitabu hiki kwa haki hali ya kuwa ni chenye kusadikisha yaliyo kuwa kabla yake katika vitabu na kuyalinda)) [Al-maaida:48]

س ٤٦: ما اليوم الآخر؟

S46: Ni ipi siku ya mwisho?

ج ٤٦: هو يوم القيامة الذي يبعث الناس فيه للحساب والجزاء.

J46: Ni siku ya Kiyama (kisimamo) ambayo watafufuliwa watu katika siku hiyo kwa ajili ya kuhesabiwa na kulipwa.

س ٤٧: ما حكم الإيمان باليوم الآخر؟

S47: Ni ipi hukumu ya kuamini siku ya mwisho?

ج ٤٧: واجب لا يقبل الإيمان إلا به

J47: Ni wajibu (lazima), haitokubaliwa imani isipokuwa kwa kuamini Imani hiyo.

س ٤٨: ما معنى الإيمان بالقدر؟

S48: Nini maana ya kuamini Qadari?

ج ٤٨: القدر: هو تقدير الله للمخلوقات حسبها سبق به علمه واقتضته حكمته.

J48: **Qadar**: ni makadirio ya Allah kwa viumbe wake kulingana na ilivyotangulia elimu yake, na ikahukumu hekima yake.

س ٤٩: ما حكم الإيمان بالقدر؟

S49: Ni ipi hukumu ya kuamini Qadar?

ج ٤٩: واجب لا يقبل الإيمان إلا به.

J49: Ni wajibu (lazima), haitokubaliwa imani isipokuwa kwa kuamini Imani hiyo.

س ٥٠: ما الإحسان؟

S50: Ni nini ihsani?

ج ٥٠: الإحسان: هو أن تعبد الله كأنك تراه، فإن لم تكن تراه فإنه يراك.

J50: **Ihsani**: ni kumuabudu Allah kama vile unamuona, kwani ikiwa wewe humuoni hakika yeye anakuona.

س ٥١: ما تعريف الرياء؟

S51: Nini maana ya Riya (kujionesha)?

ج ٥١: الرياء: هو أداء العبادة من أجل أن يراه الناس ويمدحوه.

J51: *Riya* ni mtu kutekeleza ibada ili watu wamuone na wamsifu.

س ٥٢: ما حكم الرياء؟

S52: Nini hukumu ya Riya?

ج ٥٢: الرياء محرم وهو من الشرك الأصغر. والدليل قول النبي عليه الصلاة والسلام: « أخوف ما أخاف عليكم الشرك الأصغر » فستل عنه فقال: ((الرياء)). رواه أحمد وصححه الألباني.

J52: Riya ni haramu na ni katika shirki ndogo. Na dalili ni kauli ya Mtume ﷺ: (Jambo lenye kuogopesha zaidi ambalo naliogopea kwenu ni shirki ndogo, akaulizwa kuhusu hio (shirki ndogo) akasema: (Riya)). (Ameipokea Ahmad na amesahihisha Albaniy).

س ٥٣: من نبيك؟

S53: Ni nani Nabii wako?

ج ٥٣: نبيي هو محمد بن عبد الله بن عبد المطلب بن هاشم، وهاشم من قريش، وقريش من كنانة، وكنانة من العرب، والعرب من ذرية إسماعيل وإسماعيل بن إبراهيم عليه الصلاة والسلام.

J53: Nabii wangu ni Muhammad bin Abdillah bin Abdil Mutwalib bin Hashim, na Hashim anatokana na Quraysh na Quraysh anatokana na Kinana na Kinana anatokana na waarabu na waarabu ni katika kizazi cha Ismail, na Ismail ni mtoto wa Ibrahim.

س ٥٤: ما أعظم دلائل نبوته؟

S54: Ni ipi alama kubwa zaidi ya Utume wake?

ج ٥٤: أعظم دلائل نبوته القرآن العظيم وهو كلام الله الذي هو الهدى والشفاء والنور .
 قال تعالى: ﴿قُلْ لِّئِنِ اجْتَمَعَتِ الْإِنْسُ وَالْجِنُّ عَلَىٰ أَنْ يَأْتُوا بِمِثْلِ هَذَا الْقُرْآنِ لَا يَأْتُونَ بِمِثْلِهِ وَلَا
 كَانَ بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ ظَهِيرًا﴾ [الإشراء : ٨٨].

J54: Alama kubwa zaidi ya utume wake ni Qur'an tukufu, nayo ni maneno ya Allah ambayo ni uongofu na ponyo na nuru. Amesema Allah mtukufu: ﴿Sema ewe Mtume lau wangekusanyika watu na majini ili walete mfano wa hii Qur'an hawatoileta hata wakisaidiana wao kwa wao﴾ [Israa: 88]

س ٥٥: ما أعظم حقوق النبي ﷺ؟

S55: Ni ipi haki kubwa zaidi ya Mtume ﷺ?

ج ٥٥: من أعظم حقوق النبي عليه الصلاة والسلام: الإيمان الصادق به عليه الصلاة والسلام، وأن الله أرسله للجن والإنس كافة، ووجوب طاعته والحذر من معصيته، واتباعه والاقتراء به، وتعظيم سنته، ومحبة ﷺ أكثر من الأهل والولد والناس أجمعين، وتوقيره واحترامه، والصلاة عليه ﷺ، وعدم الغلو فيه، ورفع فوق منزلته التي أنزله الله فيها.

J55: Miongoni mwa haki kubwa za Mtume ﷺ ni kumuamini yeye imani ya kweli na kuamini kwamba Allah anemtuma kwa majini na watu wote, na ulazima wa kumtii yeye na kutahadhari kumuasi, na kumfuata na kumuigiza na kuzitukuza sunna zake na kumpenda ﷺ zaidi kuliko mke na watoto na watu wote kwa ujumla na kumuheshimu na kumswalia ﷺ, na kutokuvuka mipaka yake na kutokumnyanyua zaidi ya daraja yake aliyomuweka Allah.

س٥٦: ما السحر؟

S56: Nini uchawi?

ج٥٦: السحر: هو عمل شيطاني يؤثر في القلوب والأبدان حقيقة، ومنه تخيلات تؤثر في الأبصار لا حقيقة لها.

J56: *Uchawi* ni amali za kishetani ambazo zinaathiri katika nyoyo na viwiliwili kwa uhakika, na upo katika uchawi ambao ni wa kudanganya unaoathiri machoni wala hauna uhakika.

س٥٧: ما الكهانة؟

S57: Nini ukuhani?

ج٥٧: الكهانة هي: ادعاء علم الغيب بواسطة استخدام الجن.

J57: *Ukuhani* ni kudai kujua elimu ya ghaibu kwa kupitia majini.

س٥٨: من العراف؟

S58: Ni nani Arrafu?

ج٥٨: العراف: هو الذي يدعي معرفة الأمور الغيبية بمقدمات يستدل بها على المسروق ومكان الضالة. وقيل: العراف اسم للكاهن والمنجم والرمال ونحوهم ممن يتكلم في معرفة الأمور الغيبية بواسطة الجن. ومن أعمالهم التنجيم وقراءة الكف والفرجان والاستدلال بهذه الأشياء على الأمور الغيبية.

J58: *Arrafu* ni yule anaedai kuyajua mambo ya ghaibu kwa vitangulizi, (hudai) kufahamu vitu vilivyo ibiwa na sehemu ya kitu kilichopotea. Na imesemwa kuwa: *Arrafu* ni jina la kuhani na mtizamia nyota na mpiga ramli na mfano wao, katika wale wanaozungumzia kujua mambo ya ghaibu kupitia majini, na miongoni mwa amali zao ni kutizamia nyota, kusomea

kiganja na kwenye kikombe na kutaka kujua mambo ya ghaibu (yaliyofichikana) kupitia vitu hivyo.

س ٥٩: ما حكم الذهاب للعراف والكاهن وغيرهما ممن يدعي معرفة علم الغيب؟

S59: Nini hukumu ya kwenda kwa *Arrafu* na kuhani na wengineo katika wale wanaodai kujua elimu ya ghaibu?

ج ٥٩: يحرم الذهاب إلى الساحر والعراف والكاهن ففي (صحيح مسلم) قول النبي ﷺ: «من أتى عرافا فسأله عن شيء، لم تقبل له صلاة أربعين ليلة». وعن أبي هريرة رضي الله عنه عن النبي ﷺ قال: «من أتى عرافا أو كاهنا فصدقه فيما يقول، فقد كفر بما أنزل على محمد ﷺ». رواه أحمد وأبو داود والترمذي.

J59: Ni haramu kwenda kwa mchawi, *arrafu* na kuhani, (imekuja) katika Sahihi ya Muslim kauli ya Mtume ﷺ: ((Atakaye muendea *arrafu* na akamuuliza kitu chochote haikubaliwi swala yake siku arobaini)). Na kutokana na Abu Hurayra (radhi za Allah ziwe juu yake) kutoka kwa Mtume ﷺ amesema: ((Atakae muendea *arrafu* au kuhani na akamuamini kwa anayoyasema basi amekufuru yote yaliyoshushwa kwa Muhammad ﷺ)). [ameipokea Ahmad, Abuu Daud na Tirmidhiy].

س ٦٠: ما حكم السحر وتعلمه؟

S60: Nini hukumu ya uchawi na kujifundisha Uchawi?

ج ٦٠: السحر كله محرم وكفر، تعلمه وتعليمه، لا يباح شيء منه، قال تعالى: ﴿وَمَا كَفَرَ سُلَيْمَانُ وَلَٰكِنَّ الشَّيَاطِينَ كَفَرُوا﴾ [البقرة: ١٠٢]

J60: Uchawi wote ni haramu na ni ukafiri, kujifundisha na kuufundisha, si halali chochote katika uchawi, Amesema Allah mtukufu: ﴿ Na hajakufuru

Suleiman lakini mashetani ndio waliokufuru walikuwa wakiwafundisha watu uchawi ﴿... mpaka mwisho wa aya [Al-Baqarah 102].

س ٦١: ما حكم مطالعة أبراج الحظ والمستقبل والتصديق بها؟

S61: Nini hukumu ya kuangalia nyota za bahati na za kuagua mambo ya mbele na kuziamini?

ج ٦١: هي من أعمال أهل الجاهلية وهي داخله في تصديق العرافين والمنجمين في ادعاء علم الغيب قال ﷺ: «من اقتبس شعبة من النجوم فقد اقتبس شعبة من السحر زاد ما زاد». رواه أبو داود وإسناده صحيح.

J61: Hizo ni katika amali za watu wa *Jaahiliyah*, na hayo yanaingia katika kuwaamini waganga na watizamia nyota katika kudai kujua elimu ya ghaibu, Amesema Mtume ﷺ: ((Atakae chuma sehemu katika elimu ya nyota hakika amechuma sehemu katika uchawi atazidi [uchawi] kila atakavyo zidi [kujifunza elimu ya nyota])). [Ameipokea Abu Daud na isnadi yake ni sahihi].

س ٦٢: ما تعريف التائم؟

S62: Nini maana ya *tamaaim* (hirizi)?

ج ٦٢: التائم: جمع تيمة وهي خرزات، أو عظام أو كتابات أو سيور أو خيوط أو خرق أو غيرها تعلق في أعناق الصبيان، في العضد أو على البيوت أو السيارات بغرض دفع البلاء قبل حدوثه، أو رفعه بعد وقوعه.

J62: *Tamaaim* ni wingi wa neno "*tamimah*" nazo ni shanga au mifupa au maandishi au kanda (za viatu au za mikoba) au nyuzi au vitambaa au vyenginevyo ambavyo huning'inizwa kwenye shingo za watoto au katika *adhudi* -kijimbi cha mkono- au huning'inizwa kwenye majumba au magari

kwa lengo la kuzuia balaa kabla ya kutokea au kuondoa balaa baada ya kutokea.

س ٦٣: ما حكم التهايم؟

S63: Nini hukumu ya hirizi?

ج ٦٣: شرك أصغر وقد تكون شركا أكبر إذا اعتقد أنها تنفع أو تضر من دون الله. والدليل قوله عليه الصلاة والسلام: « من علق تميمة فقد أشرك ». رواه أحمد وصححه الألباني.

J63: Ni shirki ndogo na inaweza kuwa ni shirki kubwa ikiwa mtu ataitakidi kwamba hirizi inanufaisha au inadhuru kinyume na Allah. Na dalili ni kauli yake Mtume ﷺ: ((Atakae ning'iniza hirizi hakika amefanya shirki)). [Ameipokea Ahmad na ameisahihisha Albaniy].

س ٦٤: ما الرقى الشرعية وما حكمها؟

S64: Ni zipi ruqyah za kisheria na nini hukumu yake?

ج ٦٤: هي القراءات على المريض من القرآن أو الأدعية والنفث على موضع الألم. والرقية جائزة قال ﷺ: « لا بأس بالرقى ما لم تكن شركا ». رواه مسلم. ويشترط لجوازها أن تخلو من الشرك وأن يعتقد أنها لا تؤثر بذاتها، بل هي سبب والنفع والضرر بيد الله سبحانه وأن تكون باللسان العربي أو بما يعرف معناه من غيره وأن تكون بكلام الله وبأسمائه وصفاته.

J64: Ni kumsomea mgonjwa sehemu ya Qur'an au dua na kupuliza sehemu yenye maumivu, na ruqyah inafaa, amesema Mtume ﷺ ((Haina tatizo ruqya ikiwa haijawa shirki)). [Ameipokea Muslim]. Na ili ruqya ifae, ni sharti iepukane na shirki na iaminiwe kuwa ruqyah haiathiri yenyewe, bali ni sababu tu na madhara na manufaa yapo mkononi mwa Allah mtukufu, na iwe ruqyah kwa lugha ya kiarabu, au kwa maneno yanayofahamika maana

yake katika lugha nyengine (isiyokuwa ya kiarabu), na iwe ruqyah ni kwa maneno ya Allah na majina yake na sifa zake.

س٦٥: ما الطيرة؟

S65: Nini mkosi?

ج٦٥: الطيرة: هي التفاؤل أو التشاؤم بالطيور.

J65: Mkosi ni kutarajia mambo mazuri au kukhofia mambo mabaya kwa kupitia ndege.

س٦٦: ما حكمها؟ مع الدليل.

S66: Nini hukumu yake? Pamoja na dalili.

ج٦٦: محرمة وهي من الشرك الأصغر وقد تكون شركا أكبر إذا اعتقد أنها تنفع أو تضر من دون الله والدليل قوله عليه الصلاة والسلام: « الطيرة شرك ». رواه أحمد وأبو داود.

J66: Ni haramu, nayo ni katika shirki ndogo na inaweza kuwa ni shirki kubwa ikiwa ataitakidi kuwa mkosi unafaa au unadhuru kinyume na Allah, na dalili ni kauli yake Mtume ﷺ: ((Kuamini mkosi ni shirki)). [Ameipokea Ahmad na Abuu Daud]

س٦٧: هل تحصل الطيرة في غير الطيور؟

S67: Je kunapatikana mkosi kwa kitu kisichokuwa ndege?

ج٦٧: نعم مثل: التطير ببعض الشهور، أو الأيام أو الحيوانات أو ببعض أصحاب الصفات البدنية كالأعمى والأعرج وغيرهم.

J67: Ndio, mfano: kuamini mkosi kwa baadhi ya miezi au masiku au wanyama au kwa baadhi ya watu wenye sifa za kimwili kama kipofu, kilema -kiwete au kiguru- na wengine.

س٦٨: ما معنى الاستسقاء بالأنواء؟

S68: Nini maana ya kuomba mvua kwa kutumia nyota (*Anwaai*)?

ج٦٨: الأنواء هي النجوم. ومعنى الاستسقاء بالأنواء، أي: طلب نزول المطر من النجوم، ونسبة المطر إليها إذا نزل.

J68: *Anwaai* ni nyota. Na maana ya kuomba mvua kwa nyota ni kutaka kunyeshelazewa mvua kwa nyota na kuinasibisha mvua kwa nyota itakapo nyeshwa.

س٦٩: ما حكم الاستسقاء بالأنواء؟

S69: Nini hukumu ya kuomba mvua kwa kutumia nyota?

ج٦٩: هو على نوعين:

الأول: أن يعتقد أن النجوم هي التي تنزل المطر فهذا كفر لأنه شرك بالله سبحانه.

الثاني: أن يعتقد أن الله هو الذي يخلق المطر وينزله ولكنه يعتقد أن النجوم سبب، وهذا شرك

أصغر لأنه نسب نعمة الله إلى غيره ولإنه سبحانه لم يجعل النجوم سببا.

J69: Jambo hilo lina aina mbili:

Ya kwanza: Aitakidi kuwa nyota ndio zinazoleta mvua, aina hii ni ukafiri kwa sababu ni kumshirikisha Allah.

Ya pili: Aitakidi kwamba Allah ndiye anayeumba mvua na kuitaremsha lakini aitakidi kuwa nyota ndio sababu, na aina hii ni shirki ndogo kwa sababu amenasibisha neema ya Allah kwa mwengine asiyekuwa Allah, na kwa sababu Allah hajazifanya nyota kuwa ni sababu (ya kunyeshwa mvua).

س ٧٠: ما الدليل على تحريم الاستسقاء بالنجوم؟

S70: Ni ipi dalili juu uharamu wa kuomba mvua kwa nyota?

ج ٧٠: الدليل قول النبي ﷺ: « قال الله تعالى: من قال: مطرنا بفضل الله ورحمته فذلك مؤمن بي كافر بالكوكب وأما من قال: مطرنا بنوء كذا وكذا فذلك كافر بي مؤمن بالكوكب». رواه البخاري ومسلم.

J70: Dalili ni kauli ya Mtume ﷺ ((Amesema Allah Mtukufu: Atakayesema: Tumenyeshzewa mvua kwa fadhila za Allah na rehema zake, basi huyo ni muumini aliye niamini mimi na ni kafiri aliye zikufuru nyota, ama atakayesema: tumenyeshzewa mvua kwa nyota kadha na kadha, basi huyo ni kafiri aliye nikufuru mimi na muumini wa nyota)) [Ameipokea Bukhari na Muslim]

س ٧١: ما حكم بناء المساجد على القبور؟

S71: Nini hukumu ya kujenga misikiti kwenye makaburi?

ج ٧١: محرم، وهو وسيلة للشرك، قال رسول الله ﷺ « لعنة الله على اليهود والنصارى اتخذوا قبور أنبيائهم مساجد » رواه البخاري.

J71: Ni haramu, nayo ni njia ya kuelekea kwenye shirki, amesema Mtume ﷺ ((Laana za Allah ziwe juu ya Mayahudi na Manaswara wameyafanya makaburi ya mitume yao kuwa ni misikiti)). [Ameipokea Bukhari]

س ٧٢: ما معنى التبرك؟

S72: Nini maana ya kutabaruku?

ج ٧٢: التبرك: طلب البركة، والبركة هي حصول الخير ودوامه.

J72: Kutabaruku ni kutaka baraka, na baraka ni kupatikana kheri na kudumu hizo kheri.

س ٧٣: ما أقسام التبرك؟

S73: Ni vipi vigawanyo vya kutabaruku (kutaka baraka)?

ج ٧٣: (١) - التبرك المشروع: وهو الجائز وهو ما دلت عليه الأدلة من القرآن والسنة.

(٢) - التبرك الممنوع: وهو المحرم.

J73: 1- Kutabaruku kulikowekewa Sheria: Na huku kunafaa nako ni kule kuliko fahamishwa na dalili katika Qur'an na sunna.

2- Kutabaruku kulikokatazwa (kulikozuiliwa) nako ni haramu.

س ٧٤: ما انواع التبرك المشروع؟

S74: Ni zipi aina za Kutabaruku kunakojuzu?

ج ٧٤: التبرك المشروع نوعان:

١ - التبرك بالأشياء المادية المحسوسة كالتبرك بماء زمزم.

٢ - التبرك بالأعمال الصالحة كالصلاة والدعاء والصدقة.

J74: Kutabaruku kuliko wekewa sheria kupo kwa aina mbili:

1- Kutabaruku kwa vitu vya kimaada vyenye kuhisiwa kama vile Kutabaruku kwa kutumia maji ya Zamzam.

2- Kutabaruku kwa amali njema kama swala, dua na sadaka.

س٧٥: ما أنواع التبرك الممنوع؟

S75: Ni zipi aina za Kutabaruku kulikokatazwa?

ج٧٥: التبرك الممنوع نوعان:

- ١- ما نهت عنه الشريعة، كالنهى عن التبرك بالأصنام والأوثان.
- ٢- ما كان من الأسباب الوهمية التي لا حقيقة لها كالتبرك بذوات الصالحين أو ثيابهم أو لعابهم، أو الأشجار أو الأحجار.

J75: Kutabaruku kulikokatazwa kupo kwa aina mbili:

- 1- Kulikokatazwa na sheria, kama kukatazwa kutabaruku kwa masanamu na mizimu.
- 2- Kulikokuwa ni katika sababu za kudhaniwa ambako hakuna uhakika, kama kutabaruku kwa dhati za watu wema au nguo zao au madenda yao au kutabaruku kwa miti au mawe.

س٧٦: ما أقسام التوسل؟

S76: Ni vipi vigawanyo vya tawassul katika dua (maombi)?

ج٧٦: التوسل في الدعاء قسمان:

- ١- التوسل المشروع: وهو التوسل الذي دلت عليه الأدلة الشرعية.
- ٢- التوسل الممنوع: وهو التوسل الذي لم تدل عليه الأدلة الشرعية أو نهت عنه.

J76: Tawassul katika dua zimegawanyika sehemu mbili:

- 1- **Tawassul inayokubalika kisheria:** Nayo ni kutawassal ambako kumefahamishwa na dalili za kisheria.
- 2- **Kutawassal kulikozuiliwa kisheria:** Nayo ni ile ambayo dalili za kisheria hazijafahamisha au zimekataza kufanya tawassul ya aina hiyo.

س ٧٧: ما أنواع التوسل المشروع في الدعاء؟

S77: Ni zipi aina za tawassul zilizowekewa sheria katika maombi?

ج ٧٧: التوسل المشروع في الدعاء ثلاثة أنواع:

- ١- التوسل بأسماء الله وصفاته؛ كأن تقول: يا رحمن ارحمني.
- ٢- التوسل بالعمل الصالح كقول الله تعالى: ﴿رَبَّنَا إِنَّنَا عَامِنَّا فَاعْفِرْ لَنَا ذُنُوبَنَا وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ﴾ [آل عمران: ١٦]
- ٣- التوسل بطلب الدعاء من الرجل الصالح الحي الحاضر، كما فعل عكاشة رضي الله عنه حين طلب من النبي صلى الله عليه وسلم أن يدعو له أن يكون من السبعين ألفا الذين يدخلون الجنة بغير حساب، فقال عكاشة بن محصن: يا رسول الله، ادع الله أن يجعلني منهم، فقال رسول الله صلى الله عليه وسلم: « أنت منهم ». [متفق عليه]

J77: Kuna aina tatu za Tawassul zinazokubalika kisheria katika maombi.

1. Kutawassal kwa kupitia majina ya Allah na sifa zake, kama mtu kusema (Ewe mwingi wa rehema nirehemu).
2. Kutawassal kwa matendo mema; Mfano wa kauli ya Allah aliposema ﴿ Ewe mola wetu mlezi hakika sisi tumeamini, basi tusamehe dhambi zetu na utukinge na adhabu za moto﴾ [A'l Imran: 16]
3. Kutawassal kwa kutaka kuombewa na mtu mwema aliye hai na aliyekuwepo, kama alivyofanya Ukasha -Allah amridhie- alipotaka kwa Mtume صلى الله عليه وسلم amuombee ila awe miongoni mwa watu sabini elfu ambao wataingia Peponi bila kuhesabiwa, akasema Ukasha bin Mihswan: Ewe Mtume wa Allah, niombee kwa Allah niwe na mimi

miongoni mwa hao, akasema Mtume ﷺ : ((Wewe ni miongoni mwa hao)). [Ameipokea Bukhari na Muslim]

س٧٨: ما أنواع التوسل الممنوع في الدعاء؟

S78: Ni zipi aina za tawassul zisizokubalika katika maombi?

ج٧٨: (١) - التوسل الشركي: وهو التوسل الذي دخل في الشرك بالله؛ كالأستغاثة بالصالحين ودعائهم من دون الله؛ كقولهم: مدد يا رسول الله، أو مدد يا جيلاني.

(٢) - التوسل البدعي: وهو التوسل بطريقة لم تدل عليها الأدلة الشرعية؛ لأن التوسل

عبادة، فلا يجوز فيها شيء، إلا بدليل شرعي، ومن التوسل البدعي: التوسل بذوات الصالحين أو جاههم.

J78: (1)- **Tawassul ya kishirikina:** Nayo ni tawassul ambayo imeingia kwenye kumshirikisha Allah, kama vile kutaka uokovu kwa watu wema na kuwaomba wao kinyume cha Allah, kama kusema kwao naomba msaada ewe mtume wa Allah, au naomba msaada ewe Jailaniy - wakimkusudia sheikh Abdulqadir Al-jailaniy-.

(2)- **Tawassul ya kizushi [bidaa]:** Nayo ni kutawassal kwa kupitia njia ambazo dalili za kisheria hazijafahamisha, kwa sababu tawassul ni ibada, basi haitafaa ndani yake chochote kile isipokuwa kwa dalili za kisheria, na katika aina za tawassul za kizushi ni kutawassal kwa dhati za watu wema au kwa kupitia jaha zao (vyeo vyao).

س٧٩: ما الشفاعة التي تكون يوم القيامة؟

S79: Ni ipi shafaa (uombezi) utakao kuwa siku ya Kiyama?

ج ٧٩: هي التوسط عند الله بجلب منفعة لأحد، أو دفع مضرة عن أحد.

J79: Ni kufanya ukati na kati (kiunganishi) cha uombezi kwa Allah kwa kuleta manufaa kwa mtu fulani au kuepusha madhara kutoka kwa mtu fulani.

س ٨٠: هل تطلب الشفاعة من الأموات؟

S80: Je hutafutwa *shafaa* (uombezi) kwa wafu?

ج ٨٠: لا تطلب الشفاعة من الأموات لأن الشفاعة ملك لله وحده قال تعالى: ﴿قُلْ لِلَّهِ الشَّفَعَةُ جَمِيعًا﴾ [الرَّؤْمَرُ : ٤٤]

J80: Shafaa (uombezi) hautafutwi kwa waliokufa, kwa sababu shafaa ni milki yake Allah peke yake. Amesema Allah: ﴿Sema; Uombezi wote ni wake Allah﴾ [Zumar: 44]

س ٨١: ما شروط الشفاعة؟

S81: Ni zipi sharti za *Shafaa* (uombezi)?

ج ٨١: شروط الشفاعة اثنان:

الأول: إذن الله للشافع أن يشفع قال تعالى: ﴿مَنْ ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِنْدَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ﴾ [البَقَرَة : ٢٥٥]

الثاني: رضى الله عن المشفوع له قال تعالى: ﴿وَلَا يَشْفَعُونَ إِلَّا لِمَنِ ارْتَضَى﴾ [الْأَنْبِيَاء : ٢٨]

J81: Sharti za shafaa ni mbili:

1. Ruhusa yake Allah kwa muombezi ili aombee, amesema Allah mtukufu; ﴿Hakuna yoyote ambaye ataombea mbele ya Allah isipokuwa kwa idhini yake﴾ [Al-Baqara: 255]
2. Allah kumridhia mwenye kuombewa. amesema Allah ﴿Na hawatangulii kumuombea yeyote isipokuwa aliyeridhiwa na Allah﴾ [Al-Anbiyaa :28]

س ٨٢: لمن تكون الشفاعة؟

S82: Ni kwa nani itakuwa *shafaa*?

ج ٨٢: تكون في أهل التوحيد، والدليل قول النبي ﷺ: «أسعد الناس بشفاعتي يوم القيامة من قال: لا إلا الله خالصا من قلبه». رواه البخاري.

J82: Itakuwa kwa watu wa Tawhidi (wenye kumpwekesha Allah, na dalili ni kauli ya Mtume ﷺ: ((Watu watakao faidika zaidi na uombezi wangu siku ya Kiyama ni yule aliyesema hakuna muabudiwa wa haki ispokuwa Allah kwa ikhlasi -kutakasa- kutoka moyoni mwake)). [Ameipokea Bukhari].

س ٨٣: ما حكم من استهزأ وسخر بالله تعالى أو كتابه أو دينه أو رسوله صلى الله عليه وسلم؟

S83: Ni ipi hukumu ya atakae cheza shere na kumdharau Allah au kitabu chake au Mtume wake ﷺ?

ج ٨٣: من سخر بشيء من ذلك؛ فحكمه أنه كافر قال تعالى: ﴿قُلْ أَبِاللَّهِ وَعَآيَاتِهِ وَرَسُولِهِ كُنْتُمْ تَسْتَهْزِءُونَ ﴿٦٥﴾ لَا تَعْتَذِرُوا قَدْ كَفَرْتُمْ بَعْدَ إِيمَانِكُمْ﴾ [التوبة: ٦٥ - ٦٦]

J83: Yoyote atakae dharau chochote katika hivyo, basi hukumu yake ni kafiri. Amesema Allah mtukufu ﴿Sema; Hivi kwa Allah na aya zake na Mtume wake mnafanyia shere? Musitoe udhuru hakika mmekufuru baada ya kuamini kwenu﴾. [At-Taubah: 65-66]

س ٨٤: ما معنى الولاة والبراء؟

S84: Nini maana ya *al-walaa* na *al-baraa* (kupenda na kuchukia)?

ج ٨٤: الولاء: هو المحبة والنصرة لله ورسوله ﷺ والمسلمين.

والدليل قوله تعالى: ﴿إِنَّمَا وَلِيُّكُمُ اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَهُمْ رَاكِعُونَ ﴿٥٥﴾ وَمَنْ يَتَوَلَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا فَإِنَّ حِزْبَ اللَّهِ هُمُ الْغَالِبُونَ ﴿٥٦﴾

[المائدة: ٥٥ - ٥٦]

والبراء: هو بغض الكفر والكافرين ومعادتهم والدليل قوله تعالى: ﴿قَدْ كَانَتْ لَكُمْ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ فِي إِبْرَاهِيمَ وَالَّذِينَ مَعَهُ إِذْ قَالُوا لِقَوْمِهِمْ إِنَّا بُرَءُؤُا مِنْكُمْ وَمِمَّا تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ كَفَرْنَا بِكُمْ وَبَدَا بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ الْعَدَاوَةُ وَالْبَغْضَاءُ أَبَدًا حَتَّى تُؤْمِنُوا بِاللَّهِ وَحَدَهُ ﴿٤٤﴾﴾ [الممتحنة: ٤٤]

J84: *Al-walaa*: ni kupenda na kunusuru kwa ajili ya Allah na Mtume wake na waislam. Na dalili ni kauli yake ALLAH mtukufu: ﴿Hakika kipenzi na msaidizi wenu enyi waumini ni Allah na mtume wake na waumini ambao wanasimamisha swala na kutoa zaka, hali ya kuwa ni wanyenyekavu. Na yoyote atakayemfanya kipenzi Allah na mtume wake, na walioamini [basi atakuwa katika kundi la Allah] na hakika kundi la Allah ndilo lenye kushinda﴾ [Al-Maidah: 55-56].

Na *al-baraa*: ni kuchukua -kujitenga- na ukafiri na makafiri na kuwafanyia udui -kutokuwa na ukaribu nao- dalili ya hilo ni kauli ya Allah aliposema; ﴿Kwa hakika kimekuwepo kwenu nyinyi kiigizo chema kwa Ibrahim na wale waliokuwa pamoja na yeye, waliposema kuwaambia watu wao [wakanushaji wa Allah] sisi tume jiepusha na nyinyi na vile mnavyoviabudu kinyume na Allah, tume wakanusha nyinyi na tumekataa ukafiri mlio nao, na umedhihiri uadui na machukivu ya milele baina yetu sisi na nyinyi muda ambao mko kwenye ukanushaji wenu, mpaka mumwamini Allah peke yake﴾ [Al-Mumtahinah: 4]

س ٨٥: ما حكم تهنئة الكفار بأعيادهم مثل عيد الكريسمس؟

S85: Ni ipi hukumu ya kuwapongeza makafiri katika sikukuu zao, mfano wa sikukuu ya Krismasi?

ج ٨٥: قال الشيخ ابن العثيمين رحمته الله: [تهنئة الكفار بعيد الكريسمس] أو غيره من أعيادهم الدينية؛ حرام بالاتفاق، كما نقل ذلك ابن القيم رحمته الله في كتابه (أحكام أهل الذمة) فتاوى ابن عثيمين (٤٤/٣).

J85: Amesema Sheikh Ibnu Uthaimin -Allah amrehemu-: “Kuwapongeza makafiri kwa sikukuu ya Krismasi au mfano wake katika sikukuu zao za kidini ni haramu kwa makubaliano ya wanachuoni, kama ambavyo alivyonukuu hilo Ibnul Qayyim -Allah amrehemu- katika kitabu chake (Ahkamu Ahli dhimmah)” Fatawa Ibnu Uthaimin (3/44).

س ٨٦: عرف البدعة؟

S86: Elezea maana ya bidaa (uzushi)?

ج ٨٦: هي التعبد لله بما لم يكن عليه الرسول صلى الله عليه وسلم وأصحابه رضي الله عنهم.

J86: Ni kumuabudia Allah kwa lile ambalo hakuwa nalo Mtume صلى الله عليه وسلم na maswaba zake -Allah awaridhie-.

س ٨٧: ما حكم البدعة في الدين؟

S87: Ni ipi hukumu ya bidaa katika dini?

ج ٨٧: محرمة، وهي من أشد المعاصي. قال رسول الله صلى الله عليه وسلم «إن خير الحديث كتاب الله وخير الهدي هدي محمد صلى الله عليه وسلم وشر الأمور محدثاتها وكل بدعة ضلالة». رواه مسلم.

J87: Ni haramu, nayo ni katika maasi makubwa. Amesema Mtume صلى الله عليه وسلم ((Hakika ya maneno bora ni kitabu cha Allah, na muongozo bora ni

muongozo wa Mtume ﷺ, na ubaya wa mambo ni mambo yenye kuzushwa, na kila kilichozushwa ni upotevu)). [Ameipokea Muslim].

س ٨٨: هل يوجد في الإسلام بدعة حسنة؟

S 88: Je katika Uislamu kuna bidaa nzuri?

ج ٨٨: لا يوجد في الإسلام بدعة حسنة. قال رسول الله ﷺ «كل بدعة ضلالة». رواه مسلم.

J88: Hakuna katika Uislamu uzushi mzuri, amesema Mtume ﷺ ((kila uzushi ni upotevu)). [Ameipokea Muslim]

س ٨٩: ما الموقف من أهل البدعة؟

S89: Ni upi msimamo wa kuwachukulia watu wa bidaa?

ج ٨٩: الواجب الحذر من أهل البدع، والتحذير منهم، وترك مجالستهم والنظر في كتبهم؛ قال ابن

عباس رضي الله عنه: (لا تجالس أهل الأهواء؛ فإن مجالستهم ممرضة للقلوب). الإبانة (٢/٤٣٨).

قال الإمام البغوي رحمته الله تعالى: (وقد مضت الصحابة والتابعون وأتباعهم وعلماء السنن على

هذا مجمعين متفقين على معاداة أهل البدع ومهاجرتهم). شرح السنة: (١/١٢٧).

J89: Ni lazima kuwa na tahadhari na watu wa bidaa, na kuwatahadharisha watu kutokana na wao, na kuacha kukaa nao na kuangalia vitabu vyao; Amesema Ibnu Abbas -Allah amridhie yeye na baba yake- “Usikae na watu wa bidaa, kwani kukaa nao ni kwenye kutia maradhi nyoyo” Al-ibana (2/438).

Akasema Imamu Baghawiy -Allah amrehemu- “Hakika wamepita maswahaba na wanafunzi wao, na waliofuata baada yao, pamoja wanachuoni wa Sunnah juu ya makubaliano na maafikiano ya kuwafanyia uadui watu wa bidaa na kuwahama”. Sharhu assunnah (1/127).

س ٩٠: ما حكم ترك الصلاة؟

S90: Ni ipi hukumu ya kuacha swala?

ج ٩٠: ترك الصلاة كفر؛ لحديث جابر رضي الله عنه قال: قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: « إن بين الرجل وبين الشرك والكفر ترك الصلاة ». أخرجه مسلم.

J90: Kuacha swala ni ukafiri, kwa hadithi ya Jabir -Allah amridhie- alisema: Amesema mtume ﷺ ((Hakika tofauti iliyopo kati ya mtu na ushirikina na ukafiri ni kuacha swala)). [Ameipokea Muslim]

س ٩١: ما حكم تكفير المسلمين بغير حق؟

S91: Ni ipi hukumu ya kuwakufurisha Waislam pasina haki?

ج ٩١: محرم، وهو من أشد الذنوب، قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: « أيما رجل قال لأخيه: يا كافر؛ فقد باء بها أحدهما، إن كان كما قال وإلا رجعت عليه ». رواه البخاري ومسلم.

J91: Ni haramu, nayo ni katika madhambi makubwa. Amesema mtume ﷺ ((Mtu yoyote atakaye mwambia ndugu yake: Ewe kafiri; basi hakika itamstahikia (dhambi hiyo) mmoja kati yao, itakapokuwa kama alivyosema itamfika au itamrejea mwenyewe)) [Ameipokea Bukhari na Muslim]

س ٩٢: ما واجب المسلم تجاه أصحاب رسول ﷺ؟

S92: Ni upi wajibu wa Muislam upande wa maswahaba wa Mtume ﷺ?

ج ٩٢: الواجب محبتهم، واعتقاد أنهم أفضل الناس بعد الأنبياء والرسل عليهم السلام، وكف اللسان عن الكلام فيهم إلا بالذكر الحسن، ويجرم سب أحد من الصحابة،: « لا تسبوا أصحابي، فوالذي نفسي بيده لو أن أحدكم أنفق مثل أحد ذهباً؛ ما بلغ مدَّ أحدهم ولا نصيفه». رواه البخاري ومسلم.

J92: Wajibu kwa Muislam ni kuwapenda, na kuamini hakika wao ndio watu bora zaidi baada ya manabii na mitume amani iwe juu yao, na kuzuia ulimi kutokana na kuwasema isipokuwa kwa kuwataja kwa mazuri, na ni haramu kumtukana yoyote katika maswahaba. Amesema mtume ﷺ :

((Msiwatukane maswahaba zangu, naapa kwa yule ambaye nafsi yangu ipo mkononi mwake, lau mmoja wenu angetoa dhahabu mfano wa mlima wa Uhudi, asingefikia kibaba cha mmoja kati yao wala nusu yake)).
[Ameipokea Bukhari na Muslim]

س ٩٣: ما الدليل على فضل الصحابة رضي الله عنهم؟

S93: Ni ipi dalili yenye kuonesha juu ya ubora wa maswahaba?

ج ٩٣: الدليل قوله تعالى: ﴿ وَالسَّابِقُونَ السَّابِقُونَ الْأُولُونَ مِنَ الْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنْصَارِ وَالَّذِينَ اتَّبَعُوهُمْ بِإِحْسَانٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ وَأَعَدَّ لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ذَلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴾ [التَّوْبَةُ : ١٠٠]

J93: Dalili ni tamko lake Allah ﴿ Na waliotangulia wa mwanzo [kwenye kuamuamini Allah], ambao ni Muhajirina na Answari na wale ambao wamewafuata kwa wema katika kutafuta radhi za mola wao, Allah amewaridhia, na wao wamemridhia yeye kwa malipo mazuri aliowaandalia kwa utiifu wao wa Imani yao, amewaandalia mabustani ya pepo ambayo inapita mito chini yake, hali ya kukaa humo milele, na huko ndiko kufaulu kuliko kukubwa﴾. [At-Taubah:100]

س ٩٤: من أفضل الصحابة؟

S94: Ni Maswahaba gani walio bora zaidi?

ج ٩٤: أفضل الصحابة الخلفاء الأربعة، وهم أبو بكر الصديق، ثم عمر بن الخطاب، ثم عثمان بن عفان، ثم علي بن أبي طالب، ثم بقية العشرة المبشرين بالجنة رضي الله عنهم.

J94: Maswahaba walio bora zaidi ni Makhalifa wanne waongofu, nao ni Abu bakar Swidik, Omar bin Khatwab, Uthmani bin Afan, na Aliy bin Abi Twalib, kisha kumi waliobakia katika waliobashiriwa pepo.

س ٩٥: ما المقصود بولاية الأمور؟

S95: Nini makusdio ya *Wulaatul-umuur* (wasimamizi wa mambo)?

ج ٩٥: هم حكام المسلمين.

J95: Ni viongozi wa Waislam.

س ٩٦: ما واجب المسلمين تجاه ولاية أمرهم؟

S96: Ni upi wajibu wa Waislam kwa upande wa wasimamizi wa mambo yao?

ج ٩٦: السمع والطاعة في غير معصية الله، ونصيحتهم، والدعاء لهم، وترك القدح فيهم على المنابر، وفي المجالس، لما يُحدثُ ذلك من فتن.

J96: Ni kuwasikiliza na kuwatii katika mambo yasiyokuwa ya kumuasi Allah, kuwanasahi na kuwaombea dua, na kuacha kuwasema vibaya katika mimbari na katika vikao kwa kuwa hilo linapelekea katika fitna.

س ٩٧: ما الدليل على ذلك؟

S97: Ni ipi dalili ya hilo?

ج ٩٧: قوله تعالى: ﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولِي الْأَمْرِ مِنْكُمْ﴾

[النِّسَاءَ : ٥٩] وقول الرسول ﷺ: « الدين النصيحة، قلنا: لمن يا رسول الله قال: لله ولكتابه

ولرسوله ولأئمة المسلمين وعامتهم». رواه مسلم.

J97: Ni kauli yake Allah aliposema: ﴿ Enyi mlio amini, mtiini Allah na Mtume wake na wasimamizi wa mambo miongoni mwenu﴾ . [An-nissa: 59]

Na kauli ya Mtume ﷺ: ((Dini ni nasaha)). Tukasema; ni kwa nani ewe

Mtume wa Allah? Akasema: ((Ni kwa Allah na kitabu chake na kwa mtume wake, na kwa viongozi wa Waislam na watu wote kwa ujumla)). [Ameipokea Muslim].

س ٩٨: كيف تكون نصيحة ولاة أمور المسلمين؟

S:98: Ni vipi zinakuwa nasaha kwa viongozi wa Waislam?

ج ٩٨: تكون بالسّر، قال ﷺ: « من أراد أن ينصح لذي سلطان فلا يبيده علانية، ولكن يأخذ

بيده فيخلو به؛ فإن قبل منه فذاك، وإلا كان قد أدى الذي عليه ». رواه أحمد وغيره، وصححه

الألباني وابن باز رحمهم الله.

J98: Zinakuwa kwa siri. Amesema Mtume ﷺ: ((Yoyote atakaetaka

kumnasihi mwenye dhamana ya uongozi, basi asimnasihi waziwazi, lakini amshike mkono wake na akae naye siri, (kisha amnasihi), pindi akikubali basi ni sawa, na akikataa basi hakika ameshatimiza wajibu wake)).

[Ameipokea Imamu Ahmad na wengineo, na akaisahihisha Al-Albaniy na Ibn Baaz -Allah awarehemu-]

س ٩٩: ما واجب المسلم عند نزول الفتن؟ مع الدليل؟

S99: Ni upi wajibu wa Muislam wakati wa kutokezea fitina? Pamoja na dalili.

ج ٩٩: الواجب الابتعاد عن الفتن، ولزوم جماعة المسلمين وإمامهم، وسؤال أهل العلم الراسخين. والدليل قوله تعالى: ﴿وَإِذَا جَاءَهُمْ أَمْرٌ مِّنَ الْأَمْنِ أَوْ الْخَوْفِ أَذَاعُوا بِهِ وَلَوْ رَدُّوهُ إِلَى الرَّسُولِ وَإِلَى أُولِي الْأَمْرِ مِنْهُمْ لَعَلِمَهُ الَّذِينَ يَسْتَنْبِطُونَهُ مِنْهُمْ وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ لَاتَّبَعْتُمُ الشَّيْطَانَ إِلَّا قَلِيلًا﴾ [النساء: ٨٣]

J99: Wajibu wake ni kujiweka mbali na fitna, na kulazimiana na jamaa [umoja] wa Waislam na kiongozi wao na kuwauliza wanachuoni waliobobea katika elimu. Na dalili ni kauli yake Allah aliposema:

﴿ Na likiwajia wao jambo la amani au jambo la khofu, wanakimbilia kulitangaza, na laiti wangelirejesha kwa Mtume na kwa wenye mamlaka kati yao, wangelijua wenye kuchambua kati yao, kama si fadhila za Allah na rehma zake kwenu wangemfuata shetani isipokuwa wachache﴾ [An-Nisaa: 83].

س ١٠٠: من هم أهل السنة والجماعة؟

S100: Ni nani Ahlu sunnah wal-jamaa?

ج ١٠٠: هم المتمسكون بسنة النبي ﷺ وأصحابه، ومن تبعهم وسلك سبيلهم في الاعتقاد والقول والعمل.

J100: Ni wale walioshikamana na sunna za Mtume ﷺ na Maswahaba wake, na waliofuata na wakapita katika njia yao katika kuamini (itikadi), kauli na matendo.

وصلى الله وسلم على نبينا محمد وعلى آله وصحبه أجمعين.

Yaliyomo

UTANGULIZI WA MTUNZI WA KITABU	2
S1: Ni kwa nini tunasoma Tawhidi?	3
S2: Wapi tunachukua itikadi yetu?	3
S3: Ni ipi misingi mitatu ambayo ni wajibu juu ya kila mwanadamu kuijua, na ambayo ataulizwa katika kaburi lake?	3
S4: Ni nani mola wako?	4
S5: Kwa jambo gani umemjua mola wako?	4
S6: Yupo wapi Allah?	5
S7: Ni ipi dalili kutoka katika Qur'an juu ya kwamba Allah aliye takasika yupo mbinguni juu ya Arshi?	5
S8: Nini maana ya amekuwa juu?	5
S10: Ni ipi dalili kutoka kwenye Qur'an kwamba Allah ameumba majini na watu kwa ajili ya kumuabudu yeye?	6
S11: Nini maana ya waniabudu mimi?	6
S12: Nini Ibada?	6
S13: Nini maana ya kushuhudia ya kwamba hapana muabudiwa isipokuwa Allah?	7
S14: Nini maana ya kushuhudia kuwa Muhammad ni mjumbe wa Allah?	7
S15: Ni jambo gani kubwa ambalo Allah mtukufu ameliamrisha?	7
S16: Ni vipi vigawanyo vya Tawhidi?	8
S17: Nini maana ya Tawhidi ya ulezi (<i>Rubuubiyah</i>)?	8
S18: Nini maana ya Tawhidi ya uungu (<i>Uluuhiyah</i>)?	8
S19: Nini maana ya Tawhidi ya majina ya Allah na sifa zake?	8
S20: Taja baadhi ya aina za Ibada?	9
S21: Ni jambo gani kubwa ambalo Allah amelikataza?	9

S22: Ni zipi aina mbili za shirki?	10
S23: Ni wakati gani ilitokea shirki ya kwanza kwa watu?	10
S24: Ni ipi sababu ya kutokea shirki kwa watu wa Nuhu?	10
S26: Ni ipi hukumu ya kuwaomba maiti (wafu)?	11
S27: Je inahitajia kumuomba Allah ukati na kati (uunganishi wa kiumbe)?	12
S28: Je maiti (wafu) wanajibu dua (maombi)?	12
S29: Ni kwa ajili ya nani tunachinja na kusali?	12
S30: Ni ipi hukumu ya kuchinja na kumsujudia asiye kuwa Allah?	13
S31: Ni ipi hukumu ya kumuapia asiye kuwa Allah; mfano kumuapia Mtume ﷺ au amana au cheo au kitu chengine?	13
S32: Ni upi wajibu juu ya Muislam upande wa majina ya Allah na sifa zake?	14
S33: Ni ipi dalili kutoka kwenye Qur'an juu ya kwamba sifa za Allah hazifanani na sifa zetu?	14
S34: Ni ipi dini yako?	14
S35: Je Allah atakubali dini yoyote isiyo kuwa Uislamu baada ya kutumwa Muhammad ﷺ?	15
S36: Nini maana ya Uislamu?	15
S37: Ni zipi nguzo za Uislamu?	15
S38: Nini maana ya Imani?	16
S39: Ni zipi nguzo za Imani?	16
S40: Ni nani Malaika?	17
S41: Ni ipi hukumu ya kuamini Malaika?	17
S42: Ni nani mbora zaidi wa Malaika?	17
S43: Ni vipi vitabu vya mbinguni?	17
S44: Ni ipi hukumu ya kuamini vitabu?	18

S45: Ni kipi kitukufu zaidi katika vitabu vya mbinguni?	18
S46: Ni ipi siku ya mwisho?	18
S47: Ni ipi hukumu ya kuamini siku ya mwisho?	19
S48: Nini maana ya kuamini Qadari?	19
S49: Ni ipi hukumu ya kuamini <i>Qadar</i> ?	19
S50: Ni nini ihsani?	19
S51: Nini maana ya Riya (kujionesha)?	19
S52: Nini hukumu ya Riya?	20
S53: Ni nani Nabii wako?	20
S54: Ni ipi alama kubwa zaidi ya Utume wake?	20
S55: Ni ipi haki kubwa zaidi ya Mtume ﷺ?	21
S56: Nini uchawi?	22
S57: Nini ukuhani?	22
S58: Ni nani <i>Arrafu</i> ?	22
S59: Nini hukumu ya kwenda kwa <i>Arrafu</i> na kuhani na wengineo katika wale wanaodai kujua elimu ya ghaibu?	23
S60: Nini hukumu ya uchawi na kujifundisha Uchawi?	23
S61: Nini hukumu ya kuangalia nyota za bahati na za kuagua mambo ya mbele na kuziamini?	24
S62: Nini maana ya <i>tamaaim</i> (hirizi)?	24
S63: Nini hukumu ya hirizi?	25
S64: Ni zipi ruqyah za kisheria na nini hukumu yake?	25
S65: Nini mkosi?	26
S66: Nini hukumu yake? Pamoja na dalili.	26
S67: Je kunapatikana mkosi kwa kitu kisichokuwa ndege?	26
S68: Nini maana ya kuomba mvua kwa kutumia nyota (<i>Anwaai</i>)?	27
S69: Nini hukumu ya kuomba mvua kwa kutumia nyota?	27

S70: Ni ipi dalili juu uharamu wa kuomba mvua kwa nyota?	28
S71: Nini hukumu ya kujenga misikiti kwenye makaburi?	28
S72: Nini maana ya kutabaruku?	28
S73: Ni vipi vigawanyo vya kutabaruku (kutaka baraka)?	29
S74: Ni zipi aina za Kutabaruku kunakojuzu?	29
S75: Ni zipi aina za Kutabaruku kulikokatazwa?	30
S76: Ni vipi vigawanyo vya tawassul katika dua (maombi)?	30
S77: Ni zipi aina za tawassul zilizowekewa sheria katika maombi?	31
S78: Ni zipi aina za tawassul zisizokubalika katika maombi?	32
S79: Ni ipi <i>shafaa</i> (uombezi) utakao kuwa siku ya Kiyama?.....	32
S80: Je hutafutwa <i>shafaa</i> (uombezi) kwa wafu?	33
S81: Ni zipi sharti za <i>Shafaa</i> (uombezi)?	33
S82: Ni kwa nani itakuwa <i>shafaa</i> ?	34
S83: Ni ipi hukumu ya atakae cheza shere na kumdharau Allah au kitabu chake au Mtume wake ﷺ?	34
S84: Nini maana ya <i>al-walaa</i> na <i>al-baraa</i> (kupenda na kuchukia)?	34
S85: Ni ipi hukumu ya kuwapongeza makafiri katika sikukuu zao, mfano wa sikukuu ya Krismasi?	36
S86: Elezea maana ya bidaa (uzushi)?	36
S87: Ni ipi hukumu ya bidaa katika dini?.....	36
S 88: Je katika Uislamu kuna bidaa nzuri?	37
S89: Ni upi msimamo wa kuwachukulia watu wa bidaa?	37
S90: Ni ipi hukumu ya kuacha swala?	38
S91: Ni ipi hukumu ya kuwakufurisha Waislam pasina haki?	38
S92: Ni upi wajibu wa Muislam upande wa maswahaba wa Mtume ﷺ?	38
.....	38
S93: Ni ipi dalili yenye kuonesha juu ya ubora wa maswahaba?	39

S94: Ni Maswahaba gani walio bora zaidi?	40
S95: Nini makusdio ya <i>Wulaatul-umuur</i> (wasimamizi wa mambo)?	40
S96: Ni upi wajibu wa Waislam kwa upande wa wasimamizi wa mambo yao?	40
S97: Ni ipi dalili ya hilo?	40
S:98: Ni vipi zinakuwa nasaha kwa viongozi wa Waislam?	41
S99: Ni upi wajibu wa Muislam wakati wa kutokezea fitina? Pamoja na dalili.	42
S100: Ni nani Ahlu sunnah wal-jamaa?	42
Yaliyomo	43